BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Saba – Tarehe 20 Februari, 2025.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka 2024/2025.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

136. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Wizara na mamlaka husika zinatumia utaratibu gani katika kuijengea jamii uwezo wa udhibiti wa taka ngumu na usafi wa mazingira.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

115. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kiasi gani uzinduzi wa majengo mapya ya mahkama nne za Wilaya utarahisisha kupatikana haki kwa wananchi wa Zanzibar.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

16. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Wafanyakazi wa ndani ni miongoni mwa wafanyakazi muhimu wanaotunza nyumba na familia zetu. Kwa mujibu wa ripoti, Zanzibar inapata wafanyakazi wengi wa ndani kutoka sehemu mbali mbali za Tanzania bara kila mwaka. Hata hivyo, licha ya umuhimu wao, wafanyakazi hawa wanakabiliwa na vitendo vya unyanyasaji, mishahara midogo na vitisho kutoka kwa waajiri wao bila ya kuwa na muombezi.

(a) Kwa kuzingatia tathmini iliyofanywa na Wizara yako, ni matukio mangapi ya unyanyasaji huripotiwa na hatua gani zimechukuliwa dhidi ya waajiri.

(b) Ni sababu gani inayoifanya Serikali kushindwa kutekeleza Mkataba wa Haki za Wafanyakazi wa Ndani wa Kimataifa Nam. C189 mpaka sasa.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

105. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Kitathmini Zanzibar ina vyama vingapi vya michezo.

(b) Ni kwa utaratibu gani vyama hivi vinapata stahiki sawa kwa mujibu wa katiba zao.

183. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Hivi karibuni, Zanzibar ilipata moja katika tuzo za Kisiwa Bora cha Mahaba. Hata hivyo, watu wengi katika jamii ya Zanzibar hawakuichukulia kama ni sifa njema.

(a) Je, Serikali imeichukulia vipi tuzo hii sambamba na utunzaji wa maadili na silka za watu wa Zanzibar.

(b) Je, ni vigezo gani hutumika kuipata tuzo hii.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

26. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

    Ripoti ya tafiti ya jiolojia imebaini uwepo wa madini mbali mbali ya kimkakati hapa Zanzibar.

    Ni yepi matarajio ya Serikali katika kuhamasisha uwekezaji na ushirikishwaji wa wananchi katika soko hili jipya la ajira.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

33. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    Kuandaa vitabu mbali mbali vinavyohusu simulizi za utalii kutoka Zanzibar na kuvisambaza kwa nchi tunazolenga kupata watalii, inaweza kutoa mchango mkubwa wa kupokea watalii wengi nchini kwetu.

    Je, kwa kiasi gani Wizara yako ipo tayari kulifanyia kazi wazo hili.

34. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    Kwa kuwa nchi yetu ina utajiri mkubwa wa maumbile ya asili na maeneo ya kihistoria.

    Je, ni lini Wizara yako itaanzisha utalii wa filamu na maigizo na kuutangaza ulimwenguni.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

82. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Kiwanda cha Matrekta Mbweni kipo katika hali isiyoridhisha kutokana na uchakavu.

    Je, ni upi mpango wa Serikali wa kukikarabati au kukijenga upya kiwanda hicho.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

144. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Haiba ya mji wowote ule duniani unatambulika kutokana na usanifu wa majengo ya kisasa na yenye mvuto.

(a) Je, ni upi mpango mkakati wa kuzijenga nyumba za kisasa za makaazi katika maeneo ya Kilimani, Kikwajuni na Michenzani.

(b) Je, kwa namna gani Serikali itakamilisha mpango huo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

152. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Dhana ya kusoma ili kupata ajira Serikalini imeleta changamoto kubwa katika kutimiza ndoto za vijana wetu.

Je, ni vipi Serikali inapambana katika kuiondoa dhana hii kwenye fikra na mawazo ya vijana wetu ili kuweza kuwa na fikra mbadala.

173. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni jambo la kupongezwa kwa Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar “Zanzibar Library Services Board” (ZLSB) kwa kuanzisha na kuendeleza programu ya watoto inayoshajiisha usomaji na unawirishaji wa akili, nadhari na maarifa ya watoto.

(a) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuiimarisha programu hii.

(b) Je, Serikali inatumia utaratibu upi kuiwezesha programu hii ili iwe endelevu na inayoimarika.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

64. MHESHIMWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika upangaji wa ruti za gari za shamba, Mabaguani huwa na mchango mkubwa na hufanya kazi nzuri ya kupanga utaratibu mzuri wa zamu (tani) kwa gari hizo.

(a) Je, Serikali kupitia Wizara yako, inawatambua vipi Mabaguani hawa.

(b) Kwa kiasi gani Mabaguani huchangia pato la Serikali.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

52. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Wizara ya Uchumi wa Buluu inakabiliana vipi na viashiria vya uharibifu wa mazingira ya baharini ikiwemo utupaji wa taka za plastiki, umwagaji wa mafuta kutoka melini, umwagaji wa majitaka na kemikali za viwandani.

166. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kila ifikapo Juni 8 dunia huadhimisha siku ya bahari duniani.

Je, ni kwa kiasi gani suala la afya ya bahari yetu linazingatiwa ipasavyo.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**20 Februari, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**